**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA DARASA LA NNE 2023

## 008 DINI NA KIARABU

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO

DIBAJI ..................................................................................................... iv
1.0 UTANGULIZI ............................................................................................ 1
2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ...................................................................... 1
3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ............. 1
3.1 SEHEMU A: DINI YA KIISLAMU ............................................................ 1
3.1.1 Swali la 1: Qur-an, Tawhidi na Fiqhi ................................................ 1
3.1.2 Swali la 2. Fiqhi ............................................................................ 4
3.1.3 Swali la 3: Tawhidi na maadili ........................................................ 5
3.1 SEHEMU B: KUSOMA NA KUFAHAMU .................................................... 8
3.2.1 Swali la 4: Ufahamu ....................................................................... 9
3.2.2 Swali la 5: Nambari ....................................................................... 13
3.2.3 Swali la 6: Utungaji (التعبير) .......................................................... 15
3.2 SEHEMU C ............................................................................................ 17
3.3.1 Swali la 7: Uundaji ......................................................................... 17
3.3.2 Swali la 8: Maneno ......................................................................... 21
3.3.3 Swali la 9: Maneno ......................................................................... 22
4.0 HITIMISHO ............................................................................................ 25
5.0 MAPENDEKEZO ...................................................................................... 25
VIAMBATANISHO ........................................................................................ 26

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Darasa la Nne kwa somo la Dini na Kiarabu Mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mitihani wab Darasa la Nne ni kigezo cha miaka minne ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hupimwa ni kwa kiasi gani wameweza kufahamu masomo yao ya Darasa la Kwanza hadi la Nne. Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Msingi Juu.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii, unakusudia kuonesha tathmini juu ya majibu ya Watahiniwa katika somo la Dini na Kiarabu. Ripoti inabainisha sababu tofauti zilizosababisha watahiniwa kujibu vizuri au vibaya. Miongoni mwa sababu za watahiniwa kufanya vizuri nikuwa na ufahamu mzuri kwa mada mbalimbali zilizotahiniwa katika somo hili.

Aidha, watahiniwa walijibu vibaya kwa baadhi ya maswali kwa sababu zifuatazo, kutokuwa na uwelewa mzuri wa matakwa ya maswali, kukosa maarifa juu ya mada zilizojitokeza katika mtihani na kutokuwa na msamiati wa lugha ya Kiarabu.

Kwa kuendelea zaidi, uchamnbuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia jadweli ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti.

Kwa hiyo, imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Kiarabu katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID .A. MUKKI**

**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha ufaulu wa mtihani wa Darasa la Nne kwa somo la Dini na Kiarabu mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Taifa wa mwaka 2009 na mwaka 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Nne wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani huu ulikuwa na maswali tisa (9) yaliyogawanyika katika Sehemu A, B na C na kila sehemu ilikuwa na maswali 3. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali kama ifuatavyo. Watahiniwa waliokuwa waislamu walitakiwa kujibu Sehemu "A", Sehemu "B" ilitakiwa kujibiwa na watahiniwa waislamu na wasiokuwa wa Kislamu na Sehemu "C" ilitakiwa kujibiwa na watahiniwa waliokuwa si waislamu.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **5,834** sawa na asimia **10.39**. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia jadweli kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B na C. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa.

### 3.1 SEHEMU A: DINI YA KIISLAMU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) yaliyotokana na mada mchanganyiko kama vile; Qurani na tafsiri, Fiqhi na maadil. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la (1) lilikuwa na alama (20), swali la (2) lilikuwa na alama (15)na swali la (3) lilikuwa na alama (15). Hivyo katika sehemu hii kulikuwa na jumla ya alama (50).

#### 3.1.1 Swali la 1: Qur-an, Tawhidina Fiqhi

Swali la kwanza lilitokana na mada ya Qurani, tawhidi na Fiqhi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali hilo. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b) na kila kipengele kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) kuanzia (i) hadi (v). Kipengele (a) uchambuzi wake ni huu ufuatao:-

Kipengele cha (i) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja idadi ya herufi za idh-har ambazo ni:-

A. 1 B. 4 C. 6 D. 15

Kipengele (ii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja idadi ya aya za suratul-fiyl, ambazo ni:-.

A. 5 B. 7 C. 8 D. 9

Kipengele cha (iii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja kutaja sehemu aliyozaliwa Mtume (S.A.W).

A. Iraq B. Madiana C. Madina D. Makka

Kipengele cha (iv) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuainisha sifa za mitume ya Mwenyezi Mungu kutokana na majibu aliyotakiwa achague, ambayo no:-

A. subira na majivuno B. ukweli na uaminifu

C. upole na majigambo D. ustahamilivu na husda

Kipengele cha (v) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja sehemu iliyoteremshwa suratul-asri. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jawabu katika majibu aliyopewa kama ifuatavyo:-

A. Madina B. Maka C. Sham D. Yemen

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kulinganisha vifungu vya maneno kutoka orodha "A" na vile vinavyofanana kutoka orodha "B". Vipengele vya orodha "B" ni hivi vifuatavyo:-

A. Najisi ya kati na kati B. Mbili C. Najisi nzito

D. Najisi nyepesi E. Kinyesi F. Tatu G. Tope

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kujibu maswali yanayotokana na Qur-ani na tarekhe.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,764** sawa na asilimia **98.80** na **70** sawa na asilimia **1.20** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.


**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,850 | 32.10 | 2,314 | 40.14 | 1,600 | 27.76 | 3,914 | 67.90 |

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **40.14** upo katika kiwango cha wastani hali ambayo imepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **67.90.**

Aidha, watahiniwa **1,850** sawa na asilimia **32.10** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na maarifa mazuri juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1 (a) na (b).

**Kielelezo 1.1 (a) (Kibaya)**


JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| A | C | B | D | C |

Kielelezo nambari 1.1 (a) ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya, kwa kukosa katika vipengele vyote vya majibu yake. Hii ni kwa sababu mtahiniwa hakuweza kuchaguwa jibu lililo sahihi.

**Kielelezo 1.1 (b)(Kibaya)**

**JAWABU**

| Orodha A | i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|---|
| OrodhaB | A | C | D | E | C |

Kielelezo nambari 1.1 (b) ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya, kwa kukosa katika vipengele vyote vya majibu yake. Hii ni kwa sababu mtahiniwa hakuweza kulinganisha maelezo kuhusu najisi kutoka orodha “A” na majawabu yake kutoka orodha “B”, hali ilyopelekea kfanya vibaya katika swali lake hili.

Aidha, watahiniwa **1,600** sawa na asilimia **27.76** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.2 (a) na (b)

**Kielelezo 1.2 (a) (kielelezo kizuri)**

**JAWABU**

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| C | A | D | B | B |

Kielezo nambari 1.2 (a) ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri kipengele hiki. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu na uelewa mzuri juu ya alichoulizwa kiasi ambacho ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi wake.

**Kielelezo 1.2 (b) (kielelezo kizuri)**

**JAWABU**

| Orodha A | i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|---|
| OrodhaB | C | E | F | A | D |

Kielezo nambari 1.2 (b) ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri kipengelehikipia, na kupelekea swali lake hili kufanya vizuri. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu na uelewa mzuri juu ya alichoulizwa kiasi ambacho ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

### 3.1.2 Swali la 2. Fiqhi

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) (i) na (v) na kila kipengele kilichukua alama tatu (3), na kufanya jumla ya alama kuwa kumi na tano (15). Vipengele hivi vilikuwa na kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kchagua majibu kutoka katika maneno aliyopewa. Maneno yenyewe ni:-

Sala tano, kusali, kutia nia, tohara, kupata, sita kukosa, tano

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ujuzi na maarifa ya mtahiniwa juu ya Fiqhi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,713** sawa na asilimia **97.93** watahiniwa **121** sawa na asilimia **2.07** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 1b.

**Jadweli Nambari 1b: Uchambuzu wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,896 | 50.69 | 2,503 | 43.81 | 314 | 5.50 | 2,817 | 49.31 |

Takwimu za jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **5.50** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **49.31.**

Aidha, watahiniwa **2,896** sawa na asilimia **50.69** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielezo 2.1 (kielelezo kibaya)**

2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua maneno sahihi ndani ya kisanduku.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sala tano, | kuswali, | kutia nia, | tohara, |
| kupata, | sita, | kukosa, | tano |

i. Nguzo za udhu ni tano

ii. Miongoni mwa mambo yaliyoharamu kwa mtu asiyekua na udhu ni Sita

iii. Kati ya sababu zinazopelekea kutayammamu ni Sa latano maji.


iv. Kudumisha tohara ni wajibu kwa kila muislamu.

v. Ili sala isihi ni lazima anayesali awe Kupata

Kielelezo nambari 2.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwahuyu katika kipengele cha pilialitakiwa kutaja miongoni mwa mambo yanayotengua udhu, mtahiniwa huyu katika uchaguzi wake wa maneno kachagua neon sita ambalo sio sahihi, halikadhalika na vipengele vyengine hakuwa na uchaguzi uliokuwa sahihi, hali ambayo ilipelekea kufanya vibaya swali hili.

Aidha watahiniwa **314** sawa na asilimia **5.50** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ujuzi juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.2

**Kielelezo (2.2) ( kizuri)**


2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua maneno sahihi ndani ya kisanduku.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Sala tano, | kuswali, | kutia nia, | tohara, |
| kupata, | sita, | kukosa, | tano |

i. Nguzo za udhu ni sita.

ii. Miongoni mwa mambo yaliyoharamu kwa mtu asiyekua na udhu ni kuswali.

iii. Kati ya sababu zinazopelekea kutayammamu ni kukosa maji.

iv. Kudumisha Sala tano ni wajibu kwa kila muislamu.

v. Ili sala isihi ni lazima anayesali awe tohara

Kielezo nambari 2.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu na uelewa mzuri juu ya ibada ya sala, kiasi ambacho ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

### 3.1.3 Swali la 3: Tawhidi na maadili

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) (i) na (v) na kila kipengele kilichukua alama tatu (3), na kufanya jumla ya alama kuwa kumi na tano (15).

Kipengele cha (i) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja idadi ya mitume iliyotajwa ndani ya Qur-ani.

Kipengele cha (ii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja mitume mtatu aliyotajwa ndani ya Qur-ani.

Kipengele cha (iii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuandika mambo matatu ya kigeni yanayoigwa navijana wetu ambayo hayana maadili mema.

Kipengele cha (iv) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya Ihsan.

Kipengele cha (v) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuorodhesha majina matatu ya Mwenyezi Mungu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima kumbukumbu na maarifa ya mtahiniwa juu ya tawhidi na maadili.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,741** sawa na asilimia **98.41** watahiniwa **93** sawa na asilimia **1.59** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 1c.


**Jadweli nambari 1c: Uchambuzu wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2245 | 39.11 | 1,650 | 28.74 | 1,846 | 32.15 | 3,496 | 60.89 |

Takwimu za jadweli nambari 1c zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **28.74** upo katika kiwango cha wastani, hali iliyopelekea ufaulu wa jumla kuwa wa vizuri kwa asilimia **60.89**.

Aidha watahiniwa **2,245** sawa na asilimia **39.11** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na kumbu kumbu pamoja na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo (3.1) (kibaya)**


3. Jibu maswali yafuatayo:
i. Mitume iliyotajwa katika Qur-ani ni mingapi?
thalathini
ii. Taja Mitume mitatu (3) iliyotajwa ndani ya Qur-ani tukufu.
a) muhamadi
b) maliki
c) baswiti
iii. Andika mambo matatu (3) ya kigeni yanayoigwa na vijana wetu

ambayo hayalingani na maadili mema.

a) S'awali

b) swalia mtume

c) kwena mskitini

iv. Nini maana ya Ihsan?

Ihsani n inia ya mty

v. Kwa kutumia maandishi ya Kiswahili, orodhesha majina matatu (3) ya Mwenyezi Mungu (S.W).

a) Muhamadi


b) mtume

c) malilei

Kielelezo nambari 3.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwahuyu inaonekana haukuwa na kumbu kumbu na maarifa juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kujibu swali hili kwamfani kipengele cha (v) kilmtaka kuandika majina ya Mwenyezi Mungu, hali amabayo mtahiniwa huyu alishindwa kujibu kwa ushihi, bali alibahatisha na kupelekea kukosa katika (i) na (ii) na kupata katika (iii). Hivyo kupelekea kufanya vibaya katika swali lake hili.

Aidha watahiniwa **1,846** sawa na asilimia **32.15** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.2

**Kielelezo (3.2) ( kizuri)**



3. Jibu maswali yafuatayo:

i. Mitume iliyotajwa katika Qur-ani ni mingapi?

Mitume iliyotajwa katika Qur-ani ni ishirini na tano

ii. Taja Mitume mitatu (3) iliyotajwa ndani ya Qur-ani tukufu.

a) Adam

b) Idrisa

c) Ibrahim

iii. Andika mambo matatu (3) ya kigeni yanayoigwa na vijana wetu ambayo hayalingani na maadili mema.

a) Kuvuta sigara

b) Kunywa pombe

c) Kubaka mtoto mdogo

iv. Nini maana ya Ihsan?

Ihsan ni kuvuta na subra katika jamii Ihsan -Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kama kwamba unamuona kama wewe humuoni yeye anakuona kama yeye anakuona wewe humuoni

v. Kwa kutumia maandishi ya Kiswahili, orodhesha majina matatu (3) ya Mwenyezi Mungu (S.W).

a) arahman

b) almaliki

c) alkudus

Kielezo nambari 3.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya alichoulizwa ambapo ameweza kujibu majibu yote kwa usahihi.

## 3.2 SEHEMU B: KUSOMA NA KUFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama hamsini (50) zilizogawanywa katika maswali matatu. Swali la nne ambalo lilikuwa na alama ishirini (20), swali la tano na la sita, kila moja lilikuwa na alama kumi na tano (15). Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

### 3.2.1 Swali la 4: Ufahamu

Swali la nne lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili, kipengele “a” na kipengele “b”.

Kipengele “a” kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه). Vipengele hivi vilimtaka mtahiniwa kusoma habairi aliyopewa kwa kuifahamu kisha kujibu maswali aliyoulizwa.

Kipengele “b” nacho kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه). Vipengele hivi vilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kulingana na habari aliyosoma.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,693** sawa na asilimia **97.58,** watahiniwa **141** sawa na asilimia **2.42** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.

**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 – 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,946 | 51.75 | 1,535 | 26.96 | 1,212 | 21.29 | 2,747 | 48.25 |


Takwimu za jadweli na mbari 2a zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **51.75** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **48.25.** Aidha, watahiniwa **2,946** sawa na asilimia **51.75** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1a.

**Kielelezo 4.1a (Kibaya)**




Kielelezo 4.1a ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu, bali hata alichokiandika hakifahamiki kwani alinukuu baadhi ya ibara kutoka katika habari aliyopewa na kuyaweka tu katika sehemu alizotakiwa kujibu hayo maswali.

**Kielelezo 4.1b (Kizuri)**


أ- أَيْنَ يُصَلِّيْ فَرِيْدٌ صَلَاةَ الصُّبْحِ؟ فَرِيدٌ يُصَلِّي صَلَاةَ الصُّبْحِ فِي الْمَسْجِدِ

ب- مَتَى يَذْهَبُ فَرِيْدٌ إِلَى الْمَدْرَسَةِ؟ فَرِيدٌ يَذْهَبُ إِلَى الْمَدْرَسَةِ فِي السَّاعَةِ السَّابِعَةِ إِلَّا الرُّبْعَ.

ج- مَاذَا يَفْعَلُ فَرِيْدٌ بَعْدَ صَلَاةَ الصُّبْحِ؟ بَعْدَ صَلَاةِ الصُّبْحِ يَتَنَاوَلُ الْفُطُورَ

د- لِمَاذَا فَرِيْدٌ يَنَامُ مُبَكِّرًا؟ لِأَنَّهُ يُرِيدُ أَنْ يَنَامَ مُبَكِّرًا لِيَسْتَيْقِظَ مُبَكِّرًا

هـ- أُكْتُبْ عُنْوَانًا مُنَاسِبًا لِقِطْعَةٍ سَابِقَةٍ. عُنْوَانًا مُنَاسِبًا لِقِطْعَةِ هِيَ فَرِيدٌ الْأَنْعَالِ

Kielelezo 4.1b ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vzuri swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alifahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo aliweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu.

**Kielelezo 4.1c (Kibaya)**



(ب) اِمْلَإِ الْفَرَاغَاتِ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ مِمَّا بَيْنَ الْقَوْسَيْنِ كَمَا وَرَدَ فِي الْقِطْعَةِ:

أ) يَسْتَيْقِظُ فَرِيْدٌ مِنْ ______ وَيُصَلِّيْ صَلَاةَ الصُّبْحِ فِيْ الْمَسْجِدِ. (رَاحَتِهِ – جَوْعِهِ – نَوْمِهِ)

ب) يَرْجِعُ فَرِيْدٌ مِنَ الْمَدْرَسَةِ السَّاعَةَ ______. (الْوَاحِدَةَ– الثَّانِيَةَ - الثَّالِثَةَ)

د) بَعْدَ صَلَاةِ الْعَصْرِ يَلْعَبُ فَرِيْدٌ ______ مَعَ أَصْدِقَائِهِ. (كُرَّةَ الْيَدِ – كُرَّةَ السَّلَّةِ – كُرَّةَ الْقَدَمِ)

هـ) يَتَعَلَّمُ الدِّيْنَ وَاللُّغَةَ ______ ثُمَّ يَنَامُ فِيْ اللَّيْلِ. (الْفَرَنْسِيَّةَ – الْعَرَبِيَّةَ – السَّوَاحِلِيَّةَ)

Kielelezo 4.1c ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu kwani hakuweza kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu ayopewa.

**Kielelezo 4.1d (Kizuri)**

(ب) إِمْلَإِ الْفَرَاغَاتِ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ مِمَّا بَيْنَ الْقَوْسَيْنِ كَمَا وَرَدَ فِي الْقِطْعَةِ:

أ) يَسْتَيْقِظُ فَرِيْدٌ مِنْ __نَوْمِهِ__ وَيُصَلِّيْ صَلَاةَ الصُّبْحِ فِيْ الْمَسْجِدِ. (رَاحَتِهِ – جَوْعِهِ – نَوْمِهِ)

ب) يَرْجِعُ فَرِيْدٌ مِنَ الْمَدْرَسَةِ السَّاعَةَ __الوَاحِدَة__. (الْوَاحِدَةَ– الثَّانِيَةَ - الثَّالِثَةَ)

ج) يَتَنَاوَلُ فَرِيْدٌ __الغَذَاءَ__ مَعَ أُمِّهِ وَأَبِيْهِ وَإِخْوَانِهِ. (الْعَشَاءَ– الغَذَاءَ – الْفُطُوْرَ)

د) بَعْدَ صَلَاةِ الْعَصْرِ يَلْعَبُ فَرِيْدٌ __كُرَةَ القَدَمِ__ مَعَ أَصْدِقَائِهِ. (كُرَةَ الْيَدِ – كُرَّةَ السَّلَّةِ – كُرَّةَ الْقَدَمِ)

ه) يَتَعَلَّمُ الدِّيْنَ وَاللُّغَةَ __العَرَبِيَّةَ__ ثُمَّ يَنَامُ فِيْ اللَّيْلِ. (الْفَرَنْسِيَّةَ – الْعَرَبِيَّةَ – السَّوَاحِلِيَّةَ)

Kielelezo 4.1c ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alifahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo aliweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu kujibu aliweza kuchagua majibu sahihi miongoni mwa majibu ayopewa.

### 3.2.2 Swali la 5: Nambari

Swali la tano lilitokana na mada ya nambari ambapo mtahiniwa alitakiwa kuoanisha kwa usahihi nambari alizopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (1) hadi (5).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kuoanisha kwa usahihi nambari alizopewa zilizoandikwa kwa maneno kutoka orodha "A"na nambari zinazo nasibiana kutoka orodha "B" ambazo ziliandikwa kitarakimu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo, utambuzi na maarifa ya mtahiniwa katika nambari kwa kupitia nambari alizopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,830** sawa na asilimia **99.93** na watahiniwa **4** sawa na asilimia **0.07** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.

**Jadweli nambari 2b : Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 – 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,682 | 46.00 | 1,959 | 33.61 | 1,189 | 20.39 | 3,148 | 54.00 |

Takwimu za Jadweli na mbari 2b zinaonesha kuwa asilimia ya wastani ya ufaulu wa **33.31** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wastani kwa asilimia **54.00.** Aidha, watahiniwa **2,682** sawa na asilimia **46.00** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1

**Kielelezo 5.1 ( Kibaya)**


٥ . اِخْتَرِ الْكَلِمَاتِ الَّتِيْ فِيْ قَائِمَةِ "أ" بِمَا يُنَاسِبُهَا مِنَ الأَرْقَامِ الَّتِيْ فِيْ قَائِمَةِ "ب" ثُمَّ اكْتُبْ حَرْفَ الإِجَابَةِ فِيْ الصُّنْدُوْقِ.

| قَائِمَةُ "أ" | قَائِمَةُ "ب" |
|---|---|
| ١) مِائَةٌ | أ. ١٤٠ |
| ٢) مِائَةٌ وَسَبْعَةٌ | ب. ٩ |
| ٣) عَشَرَةٌ | ج. ٢٠٠ |
| ٤) مِائَةٌ وَأَرْبَعُونَ | د. ٥ |
| ٥) مِائَتَانِ | هـ. ١٠٠ |
| | و. ١٠٧ |
| | ز. ١٠ |

| قَائِمَةُ "أ" | ١ | ٢ | ٣ | ٤ | ٥ |
|---|---|---|---|---|---|
| قَائِمَةُ "ب" | F | A | D | G | C |

Kielelezo nambari 5.1 mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kuoanisha kwa ushihi nambari alizotakiwa kuoanisha baina ya nambari zilizoandikwa kitarakimu kutoka orodha “A” na zile zilizoandikwa kimaneno kutoka orodha “B” katika kila kipengele cha swali husika. Hali ambayo inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa mzuri juu ya mada husika.

**Kielelezo 5.2 ( Kizuri)**

٥ . اِخْتَرِ الْكَلِمَاتِ الَّتِيْ فِيْ قَائِمَةِ "أ" بِمَا يُنَاسِبُهَا مِنَ الأَرْقَامِ الَّتِيْ فِيْ قَائِمَةِ "ب" ثُمَّ اكْتُبْ حَرْفَ الإِجَابَةِ فِيْ الصُّنْدُوْقِ.

| قَائِمَةُ "أ" | قَائِمَةُ "ب" |
|---|---|
| ١) مِائَةٌ | أ. ١٤٠ |
| ٢) مِائَةٌ وَسَبْعَةٌ | ب. ٩ |
| ٣) عَشَرَةٌ | ج. ٢٠٠ |
| ٤) مِائَةٌ وَأَرْبَعُونَ | د. ٥ |
| ٥) مِائَتَانِ | هـ. ١٠٠ |
| | و. ١٠٧ |
| | ز. ١٠ |

| قَائِمَةُ "أ" | ١ | ٢ | ٣ | ٤ | ٥ |
|---|---|---|---|---|---|
| قَائِمَةُ "ب" | ه | و | ز | أ | ج |

Kielelezo nambari 5.2 mfano wa mtahiniwa aliyeweza kuoanisha kwa ushihi nambari alizotakiwa kuoanisha baina ya nambari zilizoandikwa kitarakimu kutoka orodha “A” na zile zilizoandikwa kimaneno kutoka orodha “B” katika kila kipengele cha swali husika. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada husika.

### 3.2.3 Swali la 6: UTUNGAJI (التعبير)

Swali la sita lilitokana na mada ya utungaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali aliyoulizwa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujielezea kwa mujibu wa maswali aliyoulizwa katika kila kipengele cha swali husika.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kujielezea kwa usahihi na kutumia uandishi sahihi unaozingatia kanuni za uandishi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **5,224** sawa na asilimia **89.54** na watahiniwa **610** sawa na asilimia **10.46** hawakujibu swali husika.


Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2c.

**Jadwelinambari 2c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3 .5- 9 | | 9.5 – 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 3,765 | 72.07 | 1,245 | 23.83 | 214 | 4.10 | 1,459 | 27.93 |


Takwimu za Jadweli na mbari 2c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **72.07** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **27.93.** Aidha, watahiniwa **3,765** sawa na asilimia **72.07** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu yawalichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo 6.1 ( Kibaya)**


٦ . أَجِبْ عَمَّا يَأْتِي:
أ- مَا اِسْمُكَ؟ Rosemary
ب- أَيْنَ تَسْكُنُ؟ 9 Nine
ج- مَا اِسْمُ مَدْرَسَتِكَ؟ Marriam
د- مَتَى تَذْهَبُ إِلَى الْمَدْرَسَةِ؟ Raymond
هـ- مَاذَا تَفْعَلُ فِي الْمَدْرَسَةِ؟ Zawadi

Kielelezo nambari 6.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa alishindwa kujieleza kwa mujibu wa maswali aliyoulizwa katika kila kipengele cha swali husika, hali ambayo inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uwezo wa kujieleza

**Kielelezo 6.2 ( Kizuri)**


٦ . أَجِبْ عَمَّا يَأْتِي:

أ- مَا اِسْمُكَ؟ اسمي جواهر محمود

ب- أَيْنَ تَسْكُنُ؟ أسكن في كوارا

ج- مَا اِسْمُ مَدْرَسَتِكَ؟ مدرستي اسمه مدرسة الأحباب

د- مَتَى تَذْهَبُ إِلَى الْمَدْرَسَةِ؟ أذهب إلى المدرسة في الساعة السابعة تماما في الصباح

هـ- مَاذَا تَفْعَلُ فِي الْمَدْرَسَةِ؟ في المدرستي أدرس لأنني أريد أن أكون طبيبة

Kielelezo nambari 6.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri kwa kuandika majibu sahihi na yaliyokidhi matakwa ya maswali aliyoulizwa katika kila kipengele cha swali husika, hali ambayo inaonesha kuwa mtahiniwa anauwezo wa kujieleza ingawa alifanya baadhi ya makosa ya kiuandi ama makosa ya kilugha.

## 3.3 SEHEMU C:

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama hamsini (50) zilizogawanywa katika maswali matatu. Swali la saba ambalo lilikuwa na alama ishirini (20), swali la nane na la tisa, kila moja lilikuwa na alama kumi na tano (15). Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

### 3.3.1 Swali la 7: Uundaji

Swali la saba lilitokana na mada ya uundaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kuunda maneno kwa mujibu wa maelekezo aliyopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili, kipengele "a" na kipengele "b".

Kipengele "a" kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) kuanzia (1) hadi (5). Vipengele hivi vilimtaka mtahiniwa kupanga herufu alizopewa katika kila kipengele cha swali "a" na kuunda maneno sahihi.

Kipengele “b” nacho kilikuwa na vipengele vidogo vitano (5) kuanzia (1) hadi (5). Vipengele hivi vilimtaka mtahiniwa kupanga maneno aliyopewa katika kila kipengele cha swali “b” na kuunda sentensi sahihi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uundaji sahihi wa maneno na sentensi kwa kuzingatia matumizi sahihi ya herufi na maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **220** sawa na asilimia **3.77** na watahiniwa **5,614** sawa na asilimia **96.23** hawakujibu swali husika.


Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari3a.

**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 – 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 158 | 71.82 | 53 | 24.09 | 9 | 4.09 | 62 | 28.18 |


Takwimu za Jadweli na mbari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **71.82** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **28.18.** Aidha, watahiniwa **158** sawa na asilimia **71.82** wamepata ufaulu mbaya.Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1

**Kielelezo 7.1a ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 7.1a kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kupanga vizuri herufi alizotakiwa kuzipanga na kuunda maneno sahihi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa mtahiniwa hakuwa na uwezo wowote wa uundaji wa maneno sahihi.


**Kielelezo 7.1b ( Kizuri)**




Kielelezo nambari 7.1b kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeweza kupanga vizuri herufi alizotakiwa kuzipanga na kuunda maneno sahihi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwezo mzuri wa uundaji wa maneno sahihi.

**Kielelezo 7.2a ( Kibaya)**






٤ - تَأْكُلِيْنَ – بُرْتُقَالًا – أَنْتِ

٥ - طَبِيْبٌ – حَامِدٌ

Kielelezo nambari 7.2a kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kupanga vizuri maneno aliyotakiwa kuyapanga na kuunda sentensi sahihi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa mtahiniwa hakuwa na uwezo mzuri wa uundaji wa sentensi sahihi.

**Kielelezo 7.2b ( Kizuri)**



ب- أَعِدْ تَرْتِيْبَ الْكَلِمَاتِ الْآتِيَةَ لِتُكَوِّنَ مِنْهَا جُمَلًا مُفِيْدَةً:

١ - الْمَدْرَسَةِ – إِلَى – أَحْمَدُ - ذَهَبَ

٢ - التِّلْمِيْذُ – الْمَاءَ – شَرِبَ

٣ - عَائِشَةُ – الدَّرْسَ – كَتَبَتْ

٤ - تَأْكُلِيْنَ – بُرْتُقَالًا – أَنْتِ

٥ - طَبِيْبٌ – حَامِدٌ

Kielelezo nambari 7.1a kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeweza kupanga vizuri maneno aliyotakiwa kuyapanga na kuunda sentensi sahihi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwezo mzuri wa uundaji wa sentensi sahihi.

### 3.3.2 Swali la 8: Maneno

Swali la nane lilitokana na mada ya aina za maneno ambapo mtahiniwa alitakiwa kujaza au kukamilisha maneno katika sehemu zilizoachwa wazi kwa kuzingatia umoja, uwili na wingi. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa mujibu wa maelekezo aliyopewa katika kila kipengele cha swali husika.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika aina za maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **215** sawa na asilimia **3.69** na watahiniwa **5,619** sawa na asilimia **96.31** hawakujibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.

**Jadweli nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 – 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 175 | 81.40 | 37 | 17.21 | 3 | 1.39 | 40 | 18.60 |

Takwimu za Jadweli na mbari 3b zinaonesha kuwa asilimia mkubwa ya ufaulu wa **81.40** upo katika kiwango cha juu ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa mbaya kwa asilimia **18.60**. Aidha, watahiniwa **175** sawa na asilimia **81.40** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya uundaji wa sentensi kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.


**Kielelezo 8.1 (Kibaya)**


٨ - أَكْمِلِ الْجَدْوَلَ الْآتِيَةَ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ:

| مُفْرَدٌ | مُثَنًّى | جَمْعٌ |
|---|---|---|
| أ - رَجُل | | |
| ب- | بِنْتَانِ | |
| ج - | | بُيُوتٌ |
| د - بَابٌ | | |
| هـ - | قَلَمَانِ | |

Kielelezo 8.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kufanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakuwa na uwezo mzuri wa uelewa wa maneno katika hali ya umoja, uwili na wingi. Hivyo hakuweza kujibu kama alivyotakiwa.

**Kielelezo 8.2 (Kizuri)**


٨ ـ أَكْمِلِ الْجَدْوَلَ الْآتِيَةَ بِوَضْعِ كَلِمَةٍ مُنَاسِبَةٍ:

| جَمْعٌ | مُثَنًّى | مُفْرَدٌ |
|---|---|---|
| رجال | رجلان | أ - رَجُلٌ |
| بنات | بِنْتَانِ | ب - بنت |
| بُيُوتٌ | بيتان | ج - بيت |
| أبواب | بابان | د - بَابٌ |
| أقلام | قَلَمَانِ | هـ - قلم |

Kielelezo 8.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyefanya vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alikuwa na uwezo mzuri wa uelewa wa aina za maneno katika hali ya umoja, uwili na wingi, kwani alijibu kama alivyotakiwa, ingawa alifanya baadhi ya makosa madogo madogo ya kiuandishi.

### 3.3.3 Swali la 9: Maneno

Swali la tisa lilitokana na mada ya majina ya kuashiria ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia majina hayo kwa mujibu wa picha alizopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ). Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vipengele hivyo vilimtaka mtahiniwa kuashiria kwa kutumia majina hayo kwa mujibu wa picha alizopewa. Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa matumizi sahihi ya kuashiria vitu kwa mujibu wa taratibu na kanuni za lugha ya kiarabu. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **216** sawa na asilimia **3.70** na watahiniwa **5,618** sawa na asilimia **96.30** hawakujibu swali husika.


Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3c.

**Jadweli nambari 3c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 – 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 203 | 93.98 | 11 | 5.09 | 2 | 0.93 | 13 | 6.02 |

Takwimu za Jadweli na mbari 3c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **93.98** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **6.02.** Aidha, watahiniwa **203** sawa na asilimia **93.98** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1


**Kielelezo 9.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 9.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa alishindwa kuashiria vizuri na kwa usahihi kwani alishindwa kutumia vizuri majina ya kuashiria aliyopewa pamoja na picha alizoekewa jambo ambalo zinaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa mzuri juu ya mada husika

**Kielelezo 9.2 ( Kizuri)**

**Kielelezo 9.2 ( Kizuri)**




Kielelezo nambari 9.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeonyesha majibu sahihi kwa kukidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa aliweza kuashiria vizuri na kwa usahihi kwani alitumia vizuri majina ya kuashiria aliyopewa pamoja na picha alizoekewa jambo ambalo zinaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada husika

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali mawili yalijibiwa vizuri, maswali matano yalijibiwa wastani na maswali mawili yalijibiwa vibaya.

Uchambuzi huu unaonesha kuwa ufaulu ili uwe mzuri na wa ufanisi unatokana na jitihada za watahiniwa wenyewe katika kufahamu matakwa ya swali husika, maarifa waliyo nayo juu ya mada husika na kuwa na uelewa mzuri wa lugha ya Kiarabu.

Pia watahiniwa wengi hawakujibu vizuri maswali kutokana na kutokuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali, kukosa maarifa juu ya mada zilizojitokeza katika mtihani, kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha ya Kiarabu, jambo ambalo liliwafanya washindwe kujieleza kwa kutumia lugha hiyo.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiarabu na kutoa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali, lengo likiwa ni kukuza elimu ya dini ya kiislamu na lugha ya Kiarabu na kufanya marekebisho ya dosari mbalimbali na kupelekea kuongeza ufaulu katika mitihani mengine inayofuata.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kupitia uchambuzi huu mapendekezo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa ili kuinua kiwango cha ufaulu:-

a) Wanafunzi wahamasishwe katika kulisoma somo la lugha ya Kiarabu kwa sababu linaweza kuwapatia fursa nyingi katika maisha yao iwapo watalifaulu vizuri.

b) Walimu watoe mazoezi mengi zaidi kwa wanafunzi ili kuwapa uwezo wa kuyaelewa na kuyajibu maswali ya mtihani kulinga na matakwa ya kila swali.

c) Wakaguzi, maafisa wa mkoa na wilaya, walimu wakuu na wakuu wa seksheni waendelee kuwasimamia walimu wa somo la Kiarabu na Dini ili kuhakikisha wanakamilisha muhtasari kwa wakati na wanatimiza kazi zao za ufundishaji ipasavyo.

d) Washauri wazidishe bidii na mkazo zaidi katika kuwapa msaada stahiki walimu ili kuhakikisha kuwa dosari za ufundishaji zinapatiwa utatuzi madhubuti hasa kwa zile mada ambazo ufaulu wake umebainika kuwa ni wa kiwango cha chini.

e) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kupitia Taasisi ya Elimu Zanzibar ihakikishe kuwa inaandaa na kusambaza vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi wanaosoma somo la lugha ya Kiarabu na Dini pamoja na kuwapatia walimu vitabu rejea vinavyoendana na muhtasari wa somo lenyewe.

f) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu ya Zanzibar ifanye jitihada za makusudi katika kuwapatia mafunzo walimu wa somo la lugha ya Kiarabu ikiwa ni sambamba na kulishajihisha somo hili sawa na yanavyoshajihishwa masomo mengine ya lugha kama Kiswahili na Kiingereza.

g) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Zanzibar iandae utaratibu wa kuwafunza walimu namna bora za utunzi wa maswali ili walimu hao wawe na uwezo mzuri wa kuwaandaa wanafunzi kuukabili mtihani wa Taifa.

## KIAMBATANISHO NAMBARI 1

**UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA KATIKA SOMO LA DINI na KIARABU 2023**

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Qur-ani na Fiqhi | **1** | 67.90 | **VIZURI** |
| 2 | Tawhidi na Maadili | **3** | 60.89 | **VIZURI** |
| 3 | Nambari | **5** | 54.00 | **WASTANI** |
| 4 | Fiqhi | **2** | 49.31 | **WASTANI** |
| 5 | Ufahamu | **4** | 48.25 | **WASTANI** |
| 6 | Uundaji | **7** | 28.18 | **WASTANI** |
| 7 | Utungaji | **6** | 27.93 | **WASTANI** |
| 8 | Aina za Maneno | **8** | 18.60 | **VIBAYA** |
| 9 | Majina ya Kuonesha | **9** | 6.02 | **VIBAYA** |